

Mkuu wa mkoa wa Kegera, Marco Gaguti (aliyechuchumaa mweye shati jeupe) baada ya kuzindua msimu wa kahawa.

# Wakulima wa kahawa wanavyopoteza

Inatoka Uk. 9

kulinganisha na miaka ya nyuma kwa maelezo kwamba mengi yameingia kwenye mikono isiyojali ufanisi kupitia kilimo hicho.

Yapo pia madai kwamba wapo warithi walioendelea kushikilia mashamba ya kahawa kama mapambo lakini hawazalishi chochote, baadhi kwa sababu zisizoeleweka, kushindwa kuanzisha mashamba mapya au kushindwa 'kurengeta' mikahawa yao ili irudi kisasa.

Hata hivyo, uimara wa vyama vya ushirika unatajwa kuwa kitu muhimu sana katika kukuza zao la kahawa mkoani Kagera. Mkoa huu unaundwa na vyama vikuu viwili vya ushirika; Chama cha Ushirika Karagwe (KDCU) na Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Kagera (KCU 1990 LTD).

Vyama hivyo vinaundwa na vyama vya msingi zaidi ya 300 vinavyotoa huduma ya ushirika ikiwemo kukusanya kahawa za wakulima wa ushirika.

Inaelezwa kwamba miaka ya nyuma vyama vikuu vya ushirika vilifanya miradi ya maendeleo iliyochangiwa na faida iliyotokana na kilimo cha kahawa mkoani Kagera, ikiwemo kusomesha watoto wa wanachama, kujenga shule, kujenga hoteli za hadhi na kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Takwimu zilizopo zinaonesha kwamba mwaka 2019/2020 mkoa wa Kagera ulizalisha kahawa safi tani 29,000 tu kutoka kwa wakulima zaidi ya 150,000.

Mtafiti mwandamizi kutoka taasisi ya Utafiti wa Kilimo cha Kahawa Kanda ya Kagera (TACRI), Dk Nyabisi Ng'oma anasema mkoa wa Kagera unapoteza zaidi ya tani 33,000 za kahawa safi kila mwaka kutokana na kushindwa kuendesha kilimo cha kisasa.

Anasema kwa sasa miche mingi ya kahawa hasa kwa wakulima walioshindwa kubadilisha mikahawa na kuirudisha katika upya, mche mmoja unazalisha wastani wa nusu kilo wakati mche mpya wa mbuni ulioanza kuzalisha hutoa wastani wa kilo moja na nusu ya kahawa safi kwa msimu.

Anasema kushindwa kubadili mashamba ya mibuni na kukaa nayo ndani ya miaka mingi kunapoteza mapato makubwa ya wananchi na kudumaza uchumi wa wananchi wa Kegara na Taifa kwa ujumla.

"Wengi wao wanaona ni kero kung'oa mibuni ya zamani na kupanda mipya. Miche ya kisasa isiyoshambuliwa na magonjwa inachukua miaka mitatu kuanza kuvuna na kuanzia hapo mtu atavuna kahawa nyingi mpaka miaka 10. Baada ya hapo mavuno ya kahawa yanaanza kupungua na hivyo inabidi urengete ili kurudisha mibuni yako katika upya," anasema Dk Nyabisi.

Anasema wakati wa wananchi kubadilika ni sasa kwani ipo mifano mingi kwamba wale waliobadilika wanavuna mazao ya kutosha ukilinganisha na walioshikilia mashamba ya zamani.

Anasema si rahisi mtu kubadilisha shamba zima au kung'oa mibuni yote isipokuwa kila msimu anaweza kubadili shamba kwa robo ya shamba mpaka kukamilisha shamba zima na kupata mapato mazuri baada ya wastani wa miaka mitatu hadi mitano. Café Afrika ni shirika lisilo la kiserikali ambalo limefika mkoani Kagera kwa ajili ya kushirikiana na wadau wa kahawa ili kufufua zao hilo. Mratibu wa shirika hilo mkoani Kagera, Daniel Mwakalinga, anasema shirika hilo linapanga angalau kuwafikia wakulima 22,000 kwa kuwapa elimu bora ya kilimo, uzalishaji wenye tija, na namna ya kuzalisha kahawa yenye viwango vya ubora.

Shirika hilo linaloshirikiana na wadau wa kahawa kupitia ofisi ya mkuu wa mkoa wa Kagera tayari limeanza kuandaa miundombinu ya vitalu vya kahawa, kuongeza nguvu katika uzalishaji wa miche pamoja na kusaidia wakulima kupata elimu ya kuendesha kilimo kisasa.

Hivi karibuni shirika hilo lilitoa mafunzo kwa maofisa kilimo wa wilaya pamoja na wakulima 450, kugawa vifaa ambavyo vitasaidia wakulima kupata huduma za ugani na kupandisha mavuno ya wakulima.

"Tumehakikisha kila wilaya angalau tunapata wawakilishi wa wakulima na hawa 450 waliopatikana walipitishwa na vyama vyao vya msingi, kazi kubwa watakayofanya ni kutoa elimu kwa wakulima na kuzunguka katika mashamba ya wakulima kutoa mbinu bora za kilimo," anasema Mwakalinga.

Lengo la kampuni hiyo ni kuhakikisha miaka mitano ijayo mkoa wa Kagera unakomboa angalau tani 16,000 kati ya 33,000 zinazopotea bila kuzalisha ipasavyo kupitia maboresho ya huduma za ugani.

Malengo ya wadau likiwemo shirika la Café Afrika yanaenda sambamba na matumaini ya mkuu wa mkoa wa Kagera, Marco Gaguti ambaye aliwasili mkoani Kagera mwishoni mwa mwaka 2018 na kuahidi kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo.

Mara kadhaa mkuu huyo wa mkoa amefanya ziara katika mashamba ya wakulima na kutoa motisha kwa wakulima wa kahawa wanaofanya vizuri na ambao wamebadili mashamba yao.

Wakulima wa kahawa wamekuwa wakimwita mzalendo namba moja anayefuatilia kilimo cha kahawa na kufika mwenyewe mashambani katika kujaribu kubadili fikra za wakulima.

Hivi karibuni mkuu wa mkoa wa Kagera alimtembelea mkulima aitwaye Msafiri Gabagambi, mkazi wa kijiji cha Ndama wilayani Karagwe ambaye amestaafu na kuanzisha shamba la ekari sita kwa kuamua kuondoa mikahawa ya urithi yenye miaka 80 na kupanda mikahawa mipya.

Baada ya ukaguzi wa shamba lake, Gaguti anasema kama wakulima wanataka kupata fedha nyingi wangebadilika kifikra mara moja na kubadilisha mfumo wa kilimo chao.

"Hakutakuwa na maana yoyote kama tutahubiri kilimo cha kahawa bila wakulima kubadilika. Mkoa wa Kagera una mashamba mengi ambayo hayajalimwa na wakuu wa wilaya wametenga maeneo ya kilimo ila wakulima wana hofu kuwa kama watapanda mikahawa mipya huenda mavuno yatachelewa, jambo ambalo si kweli," anasema Gaguti.

Matamanio ya mkuu huyo wa mkoa ni kuona Kagera unakuwa mkoa kinara wa kuzalisha kahawa, jambo ambalo litaongeza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Audax Katabazi (63) mkazi wa kijiji cha Kitwe, Bukoba vijijini, anasema alianza kuhudumu katika shamba la mibuni kwa kutunza kahawa tangu akiwa na umri wa miaka tisa akashirikiana na baba yake. Baada ya kufikisha miaka 17, baba yake alimpatia shamba ili aliendeleze.

Kwa miaka 20 mfululizo aliendeleza shamba hilo na baadae kukosa mavuno kabisa, huku akionywa kutokata mibuni kwa madai kwamba akipanda mibuni mipya atachelewa kupata mavuno. Hivyo anasema alikaa kwa miaka mitano bila kujihusisha na kilimo cha kahawa.

Ni miaka 15 sasa tangu Katabazi apande mibuni mipya na kwa yeye ndiye anapata mavuno mengi zaidi katika kijiji chake.

Mavuno hayo anasema yanamsaidia mengi, ikiwa ni pamoja na kusomesha watoto na kuwanunulia mashamba ambapo kila mtoto anapopata likizo anapaswa kupanda walau miche 30 ya mibuni.

"Kagera tunapoteza fedha nyingi kwa kung'ang'ania mashamba yenye mibuni ya zamani," anasema

Sania Hamadi, mkulima kutoka Bukoba Vijijini, mjane aliyerithi shamba la mume wake mwaka 2000 aliamua kubadilisha taratibu katika shamba lake tangu mwaka 2010 na kwa sasa anapata mavuno yanayostahili na anajivunia kubadilisha shamba lake.

Anasema mfumo wa kurithishana mashamba unadumaza akili za vijana kwani baadhi akili yao inakua akitegemea kurithi shamba bila kujitahidi kutumia akili zao kuboresha kilimo hicho.

Anatoa mwito kwa wakulima kuizingatia elimu inayotolewa na wataalamu kwani ikizingatiwa ipasavyo mapato yataongezeka maradufu.